ISO 9001:2015 Certified

# The Regulator

JARIDA LA KILA ROBO MWAKA LA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

Linatolewa bure

ISSN: 0856 - 8030 | TOLEO MAALUM | MACHI 2025



## Miaka minne sekta ya mawasiliano Tanzania

# Ajenda ya ukuaji

# Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
# MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
### TAASISI YENYE VIWANGO VYA ISO 9001:2015

# Kampeni ya SITAPELIKI

Baadhi ya malengo ya kimkakati kwenye Mpango Mkakati wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ni kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano yenye ufanisi, ya uhakika na imara na matumizi yake kuendelezwa.

Vilevile ni kuhakikisha kuwa utendaji na ufanisi huduma zinazosimamiwa na ulinzi wa wadau vinaendelezwa na kuimarishwa.

TCRA na watoa huduma za mawasiliano wanaendesha kampeni ya elimu kuhusu namna ya kujilinda dhidi ya ulaghai mitandaoni. Kaulimbiu ya kampeni hiyo ni "SITAPELIKI" na malengo yake ni:

**i.** Kutoa mwongozo wa usalama mtandaoni na namna watumiaji na wananchi wanavyotakiwa kujilinda dhidi ya ulaghai.

**ii.** Kuhimizwa watumiaji na wananchi kuripoti matukio ya ulaghai kwa vyombo husika.

**iii.** Kuwakumbusha watumiaji kutumia njia rasmi za kupata huduma.

## Ujumbe wa kampeni

**1.** Linda taarifa zako kwa kutumia nywila (neno siri) thabiti na tofauti kwa kila akaunti.

**2.** Usifuate maelekezo na kushirikisha nywila (neno siri) au namba ya uthibitisho (OTP) yako na mtu yeyote.

**3.** Linda taarifa zako kwa kuepuka kubofya viunganishi usivyovifahamu kwenye barua pepe unazopokea. Ukipata changamoto piga namba **100** ili uhudumiwe.

**4.** Hakiki namba zako za simu ya mkononi kupitia *106#. Aidha usipokee maelekezo yoyote kwa namba usiyoifahamu.

**5.** Usiruhusu utapeli wa simu au SMS unaofanyika kimtandao. Ripoti utapeli kwenye namba 15040.

**6.** Usitekeleze maelekezo yoyote kutoka kwa mtu anayejitambulisha kuwa mtoa huduma ikiwa amekupigia kutoka namba isiyokuwa 100. Mtoa huduma wako wa mtandao wa simu atawasiliana nawe kwa namba 100 pekee. Kuwa makini.

**7.** Ukipata changamoto katika huduma ikiwemo matumizi ya data, muda wa maongezi, jumbe fupi, piga namba 100 ili uhudumiwe au fika kwenye duka la mtandao husika lililo karibu nawe.

**8.** Elewa namna kifurushi chako cha data kinavyotumika. Bofya *147*00# ili kudhibiti matumizi ya data bila kifurushi.

**9.** Kabla ya kufanya malipo au kununua bidhaa mtandaoni, hakikisha tovuti uliyoichagua inatumia itifaki salama ya Mawasiliano (HTTPS). Ikiwa huna uzoefu wa kukamilisha manunuzi mtandaoni tumia huduma ya wakala aliesajiliwa ili kukamilisha manunuzi.

**10.** Usimpe mtu mwingine taarifa zako binafsi kwenye mtandao kupitia viungo visivyojulikana au baruapepe zisizo na miadi. Wahalifu wanaweza kutumia njia hii ya kufanya utapeli, ikiwemo utapeli wa kifedha.

ISSN: 0856 - 8030
NAMBA YA USAJILI: 00000115
TOLEO MAALUM. MACHI 2025

# The Regulator

Hili ni toleo la Kiswahili la jarida la The Regulator, linalotolewa mara nne kwa mwaka na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). TCRA ni taasisi ya serikali inayosimamia mawasiliano ya kielektroniki na posta nchini. Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka.

## Sheria Na. 12 ya mwaka 2003 iliyoanzisha TCRA inaipa Mamlaka wajibu katika majukumu yafuatayo:

1. Kukuza ushindani bora na uchumi wenye tija;
2. Kulinda maslahi ya watumiaji;
3. Kulinda mitaji ya Watoa Huduma wenye ufanisi;
4. Kukuza upatikanaji wa huduma zinazodhibitiwa kwa watumiaji wote wakiwamo wenye kipato kidogo, walioko vijijini na watumiaji walio na walioko katika mazingira magumu;
5. Kuimarisha Elimu kwa Umma, uelewa na ufahamu wa huduma zinazosimamiwa na TCRA, ikiwa ni pamoja na:
   - (i) Haki na wajibu wa watumiaji na watoa huduma zinazosimamiwa;
   - (ii) Namna ya kuwasilisha malalamiko na migogoro na utaratibu wa utatuzi wake; na
   - (iii) Kazi na majukumu ya Mamlaka kwa kuzingatia umuhimu wa kulinda na kutunza mazingira.

## MKAKATI WA TCRA 2021/22-2025/26 NA MALENGO YA KIMKAKATI

Mamlaka imeandaa Malengo mbalimbali ili kufikia maono yake katika kukabiliana na mambo muhimu kama yalivyobainishwa katika uchambuzi wa hali halisi ya kisekta. Malengo hayo ni:-

1. Kukuza miundombinu na huduma za mawasiliano ya kielektroni na posta yenye usalama, ufanisi na imara;
2. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya kielektroni na posta zenye ubora na unafuu;
3. Kuimarisha ubunifu wa huduma zinazodhibitiwa, uandaaji wa maudhui ya ndani na ujanibishaji;
4. Kuimarisha ufanisi wa huduma zinazodhibitiwa na kuwalinda wadau; na
5. Kuimarisha uwezo wa taasisi.

## MATOKEO YA MKAKATI

1. Kupatikana kwa huduma za mawasiliano za uhakika na salama;
2. Kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za mawasiliano zilizo bora na nafuu;
3. Jamii yenye kuzalisha na kutumia maudhui ya ndani;
4. Kukua kwa ufanisi wa sekta ya mawasiliano na uzingatiaji wa sheria, kanuni, miongozo, kanuni ndogo na viwango kwa wadau wa sekta ya mawasiliano; na
5. Kuongezeka kwa ufanisi wa kiutendaji wa taasisi.

## SERA YA UBORA

Kutokana na nguvu za kisheria za kusimamia sekta za Mawasiliano ya Kielektroni na Posta Tanzania, TCRA imejidhatiti kuweka mazingira mazuri kwa Wenye Leseni kwa kutoa rasilimali, kudumisha na kuendelea kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Ubora ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora na nafuu kwa watumiaji ili kukidhi matakwa ya Sheria na ya kiudhibiti.

## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Mhandisi. Mwesigwa Felician

**Katibu**
Bw. Rolf Kibaja

**Wajumbe**
Bw. Semu Mwakyanjala (Mratibu)
Dkt. Philip Filikunjombe
Bw. Peter Lyimo
Bw. Robin Ulikaye
Bw. Abel John
Bi. Vitalia Kidabulo
Bw. Alpha Wawa

**Mhariri Uzalishaji**
Bw. Isaac Mruma

**Anwani ya ofisi za uhariri**
Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma,
S.L.P 474,
Postikodi 14414 Dar es Salaam.
Simu: +255 784558270, +255 784558271.
Barua pepe: regulator.magazine@tcra.go.tz;
dg@tcra.go.tz
@tcra_tanzania

# Yaliyomo

04 Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu




21 Ilani ya Uchuguzi Mkuu 2020 na Sekta ya Mawasiliano



Ripoti

08 Ajenda ya Samia yakuza sekta mawasiliano



Makala kuu

23 TCRA inavyojipambanua na mikakati ya kitaifa




Makala Maalum

19 Tanzania yaimarisha uwezo, fursa biashara ya mtandao




Dondoo

25 Takwimu sekta ya Mawasiliano



BARUA YA MHARIRI

# Malengo sekta ya mawasiliano yafikiwa na kupitwa

Toleo hili maalum linaonesha mafanikio makubwa kwenye vipaumbele 11 vya Serikali kwenye sekta ya mawasiliano kati ya mwaka 2021 na 2025.

Msukumo wa Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Rais Dkt Samia Suluhu Hassan umeshuhudia kuongezeka na kuimarishwa miundombinu na kuenea kwa huduma za simu, intaneti na utangazaji.

Tanzania inaongoza Afrika Mashariki kwa kasi ya ukuaji wa maeneo wezeshi kwenye sekta ya mawasiliano na imepita wastani wa viwango vya ukuaji Afrika kati ya mwaka 2021 na 2024. Iko mbele kwenye mawasiliano ya simu za mkononi uzao wa nne (4G), ambao umezidi kuenea kwa watu kutoka asilimia 55 mwaka 2021 hadi asilimia 88 Desemba 2024.

Teknolojia ya uzao wa tano (5G), iliyoingia Tanzania mara ya kwanza mwaka 2022, imeenea kwa asilimia 22 na kutokana na kasi yake, 5G itaongeza tija kwenye maeneo mengi. Itawezesha watumiaji wengi zaidi na vifaa vingi vyenye matumizi changamani kuunganishwa kwa wakati mmoja

Serikali imeendelea kuchukua hatua za kueneza huduma za intaneti ya kasi na yenye ufanisi sehemu nyingi. Julai mwaka huu TCRA itatoa kwa njia ya mnada masafa kwenye bendi ya 3600 hadi 3800 MHZ.

Hii ni hatua mojawapo kutekeleza mikakati ya Serikali kuongeza wigo na matumizi ya mawasiliano ya kasi, ikiwa ni pamoja watumiaji wa intaneti. Hawa waliongezeka kwa asilimia 65 kati ya Machi 2021 na Desemba 2024.

Sera nzuri na usimamizi imara vimeboresha mazingira ya ushindani, Matokeo ni kuenea kwa huduma na kushuka kwa gharama kwa hadi asilimia 58 ndani ya hii miaka minne. Serikali ya Awamu ya sita imetoa msukumo mpya kwenye matumizi ya mfumo anwani za makazi na postikodi. Mfumo huu ulitumika kikamilifu kwenye Sensa ya Watu na Makazi ya Agosti 2022.

Kuenea kwa huduma za pesa mitandaoni kumewezesha Watanzania wengi zaidi kushiriki kwenye mfumo wa fedha kidijiti. Akaunti za pesa kwa simu ziliongezeka kwa wastani wa asilimia 89.1 kati ya Machi 2021 na Desemba 2024.

Kwa upande wa posta na usafirishaji vifurushi, mipango inatekelezwa kujenga miundombinu na mifumo itakayofanikisha biashara mtandao.

Kimataifa, Tanzania imeendelea kujiimarisha kwenye sekta ya mawasiliano, na ni mjumbe wa vikao muhimu vya maamuzi vya mashirika makubwa na inaongoza kikanda kwenye maeneo mengi.




Jarida hili linakuwezesha kupitia na kupata stadi mpya na pia kupanua mtandao wako wa watu wenye weledi kama wewe. Kupata nakala za bure za jarida hili na kuwasilisha maoni, tuma barua pepe kwa

regulator.magazine@tcra.go.tz | barua@tcra.go.tz

Soma kujisajili

Tunakaribisha maoni na hoja kutoka kwa wasomaji wetu. Kwa maelezo zaidi tafadhali piga simu ya bure kwenye namba ya wateja wa TCRA, ambayo ni 0800008272.

UJUMBE WA MKURUGENZI MKUU

# Tuwe makini, tujilinde mitandaoni

***Ujumbe huu ulitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt Jabiri Bakari kwenye maadhimisho ya Siku ya Usalama Mtandaoni mwaka huu, Dodoma 11 Februari.***



Dkt. Jabiri K. Bakari, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA

Maadhimisho ya Siku ya Usalama Mtandaoni Jumanne ya pili ya mwezi Februari kila mwaka ni mpango wa kimataifa ulioanzishwa mwaka 2004 kwa lengo la kuhamasisha matumizi sahihi na salama ya mtandao wa intaneti.

Maadhimisho haya yanaunganisha mamilioni ya watu ulimwenguni kuhamasisha matumizi sahihi na salama ya mtandao na kuongeza uelewa kuhusu masuala yanayoibuka mtandaoni. Haya ni pamoja na fursa na changamoto zinazotokana na matumizi.

Kaulimbinu ya maadhimisho ya mwaka huu imewekwa kama swali  je hii ilivyo ina ukweli?  Inaongeza kwa kusisitiza umuhimu wa watumiaji wa mitandao kujilinda wao binafsi na wengine dhidi ya ulaghai na udanganyifu mtandaoni.

Kaulimbiu hii inatukumbusha umuhimu wa kuongeza umakini tunapotumia mtandao na mifumo ya teknolojia.

Hili ni muhimu katika zama hizi za taarifa; ambapo matumizi ya teknolojia za kidijiti yanakumbana na changamoto la wimbi la wahalifu mtandaoni. Hawa watumia mbinu mbalimbali, zikiwemo zinazovutia na kushawishi.

Huduma za intaneti zinakidhi mahitaji ya watumiaji kwa namna tofauti. Kwa ujumla wake zinachagiza maendeleo yao na ya nchi kwa ujumla. Ni huduma wezeshi katika ujenzi wa uchumi wa kidijiti Tanzania.

Hata hivyo, pamoja na watumiaji wengi kutumia intaneti kwa malengo chanya, kuna wachache ambao wanatumia mitandao kufanya uhalifu.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaendelea na jitihada za kulinda watumiaji na wadau wengine wa sekta ya mawasiliano.

> *Pamoja na watumiaji wengi kutumia intaneti kwa malengo chanya, kuna wachache ambao wanatumia mitandao kufanya uhalifu.*

Hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kutoa elimu endelevu kwa umma kuhusu vidokezo na mbinu za kuwa salama mtandaoni kupitia kampeni mbalimbali. Elimu hii pia inagusia kwa kina, fursa zilizopo mtandaoni ambazo kila mtumiaji anaweza kunufaika nazo.


Kwa upande wa kundi la vijana, TCRA inaratibu uanzishwaji wa vilabu vya kidijiti (Digital Clubs). Haya ni majukwaa ya hiyari yanayowaleta pamoja wanafunzi wa ngazi zote za elimu, kuanzia shule za awali hadi vyuo vikuu.

Lengo ni kukuza hamasa ya kujifunza ujuzi wa teknolojia za kidijiti na kuhamasisha ubunifu kupitia teknolojia hizo ili kuleta suluhisho kwenye changamoto mbalimbali za kijamii. Ujuzi huu pia unawaandaa vijana kushiriki kikamilifu na kunufaika na fursa zilizopo kwenye uchumi wa kijiditi.

Jitihada nyingine zinazofanywa na TCRA ni pamoja kutoa rasilimali za mawasiliano kwa wabunifu chipukizi wa TEHAMA kwa muda wa siku 90 bila malipo, ili kuweza kupima kazi na uvumbuzi wao.

TCRA pia inaratibu mashindano ya usalama mtandaoni. Mashindano haya yanawakutanisha vijana wa vyuo vikuu, kujipima uwezo wao kwenye masuala ya ulinzi wa mifumo ya teknolojia na kutoa fursa kwa vijana kuongeza ujuzi wa usalama mtandaoni, unaowawezesha kuajiriwa au kujiajiri.

Wote tunafahamu kuwa mtandao hauna mipaka ya kuzuia watu wenye nia ya kutumia vibaya kwa lengo la kujinufaisha, kwa njia ambazo sio sahihi. Njia hizo ni pamoja na ulaghai unaoweza kusababisha utapeli mtandaoni, udukuzi wa taarifa nyeti za mtu binafsi au mifumo ya teknolojia.



***Picha ya Jalada:*** *Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa Arusha wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani 8 Machi 2025.*

> ***"Hata hivyo, imebainika kuwa watumiaji wa mtandao kwa kiasi kikubwa wanachangia kufanikisha matukio mengi yanayohatarisha usalama wao mtandaoni.***

Hii ni kutokana na ama kuwa na uelewa mdogo wa matumizi sahihi ya TEHAMA au kutozingatia kanuni za kiusalama.

Hivyo iko haja ya kutoa elimu endelevu ya matumizi bora na salama ya TEHAMA na mtandao ili kuepuka athari za kiusalama.

Suala la matumizi sahihi na salama ya mtandao ni jukumu la kila mmoja wetu. Kwa muktadha huo, ni vyema kila mdau; Serikali, mashirika binafsi, Taasisi za Elimu, wanafunzi, Vyombo vya Ulinzi na Usalama, watoa huduma za mtandao na jamii kwa ujumla kushirikiana ili kuhakikisha mtandaoni ni mahali salama.

Natoa wito kwenu, kuendelea kujielimisha juu ya masuala ya mawasiliano kadri teknolojia inavyobadilika ili kuongeza weledi wa matumizi bora na salama ya huduma na bidhaa za mawasiliano ikiwemo mtandao wa intaneti.
Vilevile, natoa rai kwa washiriki wote, kufuatilia taarifa zinazotolewa na TCRA kuhusu usalama mtandaoni.

Taarifa hizi zinapatikana kwenye tovuti ya TCRA, yaani www.tcra.go.tz, kurasa za mitandao ya kijamii za Facebook, Instagram, TikTok, LinkedIn, YouTube, Threads, Podcast na chaneli ya WhatsApp kwa jina tcra tanzania.

Ninawakaribisheni kutumia vyanzo hivyo kupata taarifa mbali mbali za sekta ya mawasiliano pamoja na elimu ya matumizi salama ya mitandao na vidokezo vingine.

Ninawaomba wadau wote kuendelea kuelimisha jamii juu ya matumizi salama na sahihi ya mtandao.

MAKALA MAALUM

# Posta kwa mipango endelevu, jumuishi

***Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Dkt. Jabiri K. Bakari kwenye maadhimisho ya miaka 45 ya Siku ya Umoja wa Posta Afrika, 18 Januari 2025.***

Kauli mbiu ya mwaka huu: "Posta: Sekta Jumuishi kwa Maendeleo Endelevu ya Kijamii" inatupa hamasa ya kuboresha mawasiliano Afrika na kuhakikisha kwamba maendeleo haya yanawanufaisha wananchi wote.

Tunaposherehekea siku hii, tutafakari juu ya huduma za posta zinavyoweza kuchangia maendeleo ya jamii barani Afrika. Huduma za posta zimekuwa daraja muhimu katika kuunganisha shughuli za biashara na kijamii, kutoka kuwezesha mawasiliano hadi kuwezesha biashara na kukuza uwiano wa kijamii. Posta pia imewezesha wananchi kupata habari na huduma muhimu kwa maendeleo.

Hata hivyo, lazima tutambue kuwa kuna changamoto nyingi wakati huu wa kidijitali, kama vile usalama mitandaoni.

Changamoto hizi zinahitaji ubunifu na mabadiliko ya haraka yatakayotoa majibu. Ukuaji wa haraka wa teknolojia umebadilisha maisha ya watu kwa njia ya mawasiliano na umerahisisha ufanyaji wa biashara katika Soko la sasa linalohitaji kudumisha uaminifu.

Kipindi hiki cha mpito lazima tuhakikishe kwamba maendeleo yetu yana msingi wa uwajibikaji katika jamii.

Ili kufanikisha ajenda ya maendeleo jumuishi, lazima tuwe na kipaumbele kwenye upatikanaji wa huduma. Hii inamaanisha si tu kuongeza miundombinu ya posta ili kufikia maeneo yasiyofikika kirahisi na yasiyo na huduma za kutosha, bali pia kuhakikisha kwamba huduma za posta zinapatikana kwa bei nafuu.

Hii inahusisha huduma za uwakala za kifedha kupitia posta na huduma za kidijitali za jumuishi ambazo zinawezesha jamii zilizoko pembezoni, hivyo kuchochea uchumi wa ndani.

Mabadiliko ya huduma za posta kidijitali yamekuwa kipaumbele muhimu kutokana na kuongezeka kwa uchumi wa kidijitali. Wadau wa posta na mawakala wa usafirishaji duniani kote wanatumia teknolojia mpya ili kuboresha na kuongeza huduma zao kutokana na mahitaji ya wateja.



Uwekezaji katika teknolojia ni muhimu ili kuboresha ufanisi wa huduma na upatikanaji wake, ikijumuisha kutoa huduma za posta za kidijitali moja kwa moja au kwa kushirikiana na makampuni mengine.

Huduma hizi zinajumuisha kazi za msingi kama ufuatiliaji mtandaoni na huduma za kieletroniki za posta hadi mitandao ya serikali na biashara mtandaoni. Kukuza viwango vyenye vipimo vya usalama katika sekta ya posta ni muhimu ili kulinda wafanyakazi, mali, na vitu vinavyosafirishwa kwa njia ya posta.

Sambamba na hili ni kuhakikisha usalama wa usafiri na mfumo wa usambazaji kwa ujumla.

Ni muhimu kujua na kuelewa vitu vilivyopigwa marufuku na vinavyopaswa kudhibitiwa, kwa ajili ya usalama, ulinzi, na kufuata kanuni, ili kusaidia ukuaji wa sekta.

Kujua sheria na kuelimisha wafanyakazi na watumiaji juu ya sheria hizi kunaweza kuongeza ufanisi wa uendeshaji huku ufuatiliaji wa usalama ukidumishwa. Lazima pia tujenge ushirikiano miongoni mwa serikali, mamlaka za posta, sekta binafsi, na jamii katika kuunda mfumo thabiti wa sekta ya posta endelevu na yenye uwajibikaji kwa kijamii.

Kwa kutumia mbinu bora na kutumia nguvu zetu za pamoja, tunaweza kutatua matatizo mbalimbali ya wananchi wetu na kuondoa mipaka ya maendeleo. Zaidi ya hayo, tunapokubali ubunifu katika sekta ni lazima tuwe makini na athari za maendeleo haya katika jamii.

> ***"Ni muhimu kujua na kuelewa vitu vilivyopigwa marufuku na vinavyopaswa kudhibitiwa, kwa ajili ya usalama, ulinzi, na kufuata kanuni, ili kusaidia ukuaji wa sekta.***

Tunapaswa kuunga mkono mfumo wa posta unaothamini uadilifu, unaochochea uwazi, na unaolinda haki za watumiaji.



Sekta yenye uaminifu ni ile inayoweka ustawi wa watumiaji wake mbele, na inayohakikisha kuwa hakuna anayeachwa nyuma, hususan wale walio katika mazingira hatarishi zaidi katika jamii zetu. Tanzania tumejiandaa kukuza sekta ya posta inayowakilisha maadili haya.

Tumekaribisha mabadiliko mbalimbali yanayoimarisha ufanisi, uaminifu, na uwajibikaji wa huduma zetu za posta. Juhudi hizi si tu zinahusu kuboresha shughuli zetu, bali pia zinahusu kujenga huduma ya posta inayokuwa kichocheo cha maendeleo jumuishi katika jamii zetu.

Tunapoadhimisha Siku ya Umoja wa Posta wa Afrika, tukumbuke ahadi zetu za kujenga sekta ya posta inayowajibika kwa jamii na ambayo inakuza ushirikiano.

Kwa pamoja, tunaweza kupiga hatua siku zijazo ambapo huduma za posta hazitakuwa tu vyombo vya mawasiliano, bali zana zenye nguvu za kuendeleza matarajio ya wananchi kwa pamoja.

Ninatoa wito kwa kila mmoja wetuu kujiunga katika juhudi hizo muhimu. Tujenge motisha kwa kila mmoja, tufurahie mafanikio yetu, na tufanye kazi kwa pamoja kuendeleza maono ya pamoja ya Afrika ambapo kila raia anaweza kustawi kupitia mawasiliano ya posta.

MAKALA KUU: MIAKA MINNE YA AWAMU YA SITA (MACHI 2021 – MACHI 2025)

# Ajenda ya Samia yakuza sekta mawasiliano

Na Mwandishi wetu

Mafanikio kwenye sekta ya mawasiliano ndani na miaka minne ya uongozi wa Rais wa Awamu ya Sita Tanzania, Mh. Rais Dkt Samia Suluhu ni mengi.

Kipindi hiki kimeshuhudia maendeleo ya kasi kwenye sekta ya mawasiliano; ikiwa ni pamoja na kupanua wigo wa huduma zinazowezeshwa na teknolojia za kisasa. Serikali imeboresha sera na kanuni kadhaa ili kuhakikisha mazingira wezeshi ya ukuaji wa sekta.

Kutokana na huduma na bidhaa za mawasiliano kuwa mwezeshaji wa sekta nyingine, zinachochea kukua kwa uchumi, kuongezeka ajira, kuleta ufanisi wa utendaji na kuimarisha imani ya watumiaji wa mitandao ya mawasiliano.

Hali hii imebadili ustawi na maisha ya Watanzania na imeharakisha ujenzi uchumi wa kidijiti unaopigia chapuo zaidi duniani kwa sasa.

Miaka hii minne ya uongozi wa Rais Samia imeshuhudia ukuaji kwa viwango vinavyoifanya Tanzania ing'ae kwenye maeneo mengi kikanda na kimataifa.

Kwa sehemu kubwa mafanikio hayo yamechochewa na hatua za serikali kuendeleza miundombinu zilizochangia kuondoa tofauti kwenye mawasiliano na ripoti za hivi karibuni zinaonesha bayana namna Tanzania inavyokabili tofauti hizi.

Tofauti za kwenye mawasiliano zinatokana na kutokuwa na usawa kwenye upatikanaji, kuchukuliwa kwa matumizi na kutumika teknolojia za habari na mawasiliano (TEHAMA) na huduma kati ya maeneo na miongoni mwa watu.

Ripoti hizo ni ile ya mwaka 2024 ya Umoja wa Mawasiliano Afri-ka Mashariki (EACO) na andiko la Shirika la Mawasiliano ya Simu Ulimwenguni (ITU).




*Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa na mwanafunzi kwenye kwenye chumba cha kompyuta.*

Nyingine ni taarifa ya mwaka ya taasisi ya GSMA ambayo inasimamia maslahi ya watoa huduma za simu za mkononi duniani.

Hatua za pamoja zinazochukuliwa na wadau kwenye sekta mbalimbali pia zinachangia kupunguza tofauti za mawasiliano kidijiti. Ushiriki wa taasisi zilizo kwenye mlo-longo wa utoaji huduma za kidijiti unaopunguza gharama za kuweka miundombinu na kuiendesha.

Kwa mfano, serikali imepunguza gharama za kupitisha miundombinu kwenye hifadhi ya barabara kutoka ada ya awali na ya kila mwaka ya dola za Kimarekani 1,000 hadi 100, mtawalia.

Ada hizi zinasimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA).

MIradi ya kupelekea umeme vijijini imeondoa matatizo ya nishati kwa ajili ya televisheni, ving'amuzi na vifaa vingine vya TEHAMA. Hii ni pamoja na kuchajia simu. Umeme wa uhakika pia unawezesha watumiaji kutumia vifaa vya kis-asa zaidi kiteknolojia.

Hadi Machi 2024, asilimia 96.4 ya vijiji Tanzania Bara vilikuwa na umeme, kwa mujibu wa Wizara ya Nishati.

Sekta ya mawasiliano Tanzania inahusisha mitandao na huduma za simu na intaneti, utangaaji na posta na usafirishaji vifurushi. Ukiondoa huduma za kawaida za posta, maeneo mengine yamekuwa kwa kasi.






## Mipango kupanua wigo wa huduma

Serikali ina malengo ya kuongeza mchango wa sekta ya mawasiliano kwenye pato la Taifa kwa kuongeza matumizi ya TEHAMA. Misingi inayokidhi mahitaji ya uchumi wa kidijiti imeendelea kujengwa na kuimarishwa kwa huduma za mawasiliano. Azma ya serikali ni kuimarisha ubora wa mawasiliano nchini.

Serikali inatekeleza mradi wa kujenga minara mipya ya mawasiliano ya simu za mkononi na kuboresha iliyopo. Lengo la ujenzi na uboreshaji minara ni kuongeza nguvu ya minara kutoka 2G kwenda teknolojia za juu zaidi hadi kufikia uzao wa tano 5G.

Teknolojia ya uzao wa tano (5G), iliyoingia Tanzania mara ya kwanza mwaka 2022, imeenea miongoni mwa watu kwa asilimia 22.

Kutokana na kasi yake, 5G itaongeza tija kwenye maeneo mengi. Itawezesha watumiaji wengi zaidi na vifaa vingi vyenye matumizi changamani kuunganishwa kwa wakati mmoja.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imepanga kukamilisha mradi wa kujenga minara 758 katika kata 713 katika maeneo mbalimbali Tanzania Bara ambako hakuna mawasiliano ya uhakika. Minara 42 katika shehia 38 Unguja na Pemba umekamilika.

**Minara 758 kujengwa Tanzania Bara katika kata 713 zenye mawasiliano yasiyo na uhakika**

Ujenzi wa minara 758 ulianza mwaka 2023 na uliendа sambamba na shughuli za kuimarisha na kuongeza nguvu minara mingine 300. Lengo ni kuiwezesha kutoa huduma za intaneti ya kasi kupitia simu za mkononi na vifaa vya mkononi.

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Jerry Silaa (Mb), amesema mradi wa ujenzi wa minara hiyo ni sehemu muhimu ya mkakati wa Serikali wa kuleta mageuzi ya Kidijitali katika maeneo ya vijijini.

Zaidi ya watu milioni 8.5 waishio vijijini watafikiwa na mawasiliano mradi huo utakapokamilika ambamo kati yao milioni tatu watapata huduma za intaneti kwa mara ya kwanza.

Mradi huu unaratibiwa na kusimamiwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF). TCRA inachangia mfuko huo. Vilevile inaratibu michango ya watoa huduma.


UCSAF ina majukumu ya kufikisha huduma za mawasiliano maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara na ambayo ni vigumu kwa watoa huduma za simu kufikisha huduma za mawasiliano.

Hadi Februari 2025, UCSAF umefikisha huduma katika kata 1,582 zenye vijiji 4,396. Imejenga jumla ya minara 1,725 ambayo inatoa huduma kwa wananchi milioni 23.9.

Taarifa ya TCRA ya robo mwaka ya Oktoba-Desemba inaonesha kuwa mitambo ya kurushia mawimbi ya simu za mkononi inayowezesha 3G imefikia 12,762 na 4G imeongezeka hadi 12,562.

Mitambo kwenye minara inavyowezesha uzao wa tano, vimeongezeka kwa asilimia nane (8) na kufikia 900, ikiwa zimeenea zaidi maeneo ya mijini.

## Mikoa inayoongoza kwa vifaa vingi vya 5G Tanzania






*Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwasiliana kwa simu eneo la maafa ya jengo lililopromoka Kariakoo Dar es Salaam mwishoni mwa mwaka 2024.*

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa ingawaje mkoa wa Dar es Salaam unaongoza kwa wingi wa mitambo ya kurushia mawimbi ya mawasiliano ya 5G na ni kitovu cha mawasiliano Tanzania, Mjini Magharibi unaongoza Tanzania kwa uwiano wa laini zilizosajiliwa na mitambo.

Laini 16,097,634 zimesajiliwa Dar es Salaam na 510,853 Mjini Magharibi. Uwiano wa laini na mitambo ya 5G kwa Dar es Salaam ni 26,133 na Mjini Magharibi ni 8,807.

## Simu na intaneti

Vidokezi vya ukuaji wa sekta vinaonyesha mabadiliko ya kasi kwenye maeneo mengi. Desemba 2024 kulikuwa na laini za simu 86,847,460 ikilinganishwa na 52,885,243 Machi 2021.

Kuwepo kwa laini za simu kuzidi idadi ya watu Tanzania kunatokana na watumiaji kuwa na zaidi ya laini moja ya simu kwa sababu na matumizi mbalimbali.

Takwimu za laini zinahusisha idadi iliyotumika angalau mara moja ndani ya miezi mitatu, na sio watu wanaozitumia. Taasisi ya GSMA, inayoshughulikia maslahi ya watoa huduma za simu za mkononi ulimwenguni, inaeleza kuwa watumiaji halisi wanapatikana kwa kuigawa idadi ya laini kwa 1.8. Huu ndio wastani wa watu kumiliki laini.

Pamoja na kuongezeka kwa watu wanaofikiwa na huduma za mawasiliano ya simu za mkononi na wanaozitumia, kuna ongezeko la mashine zinazotumia laini za simu. Teknolojia ya mawasiliano baina ya vifaa vinavyojiendesha vyenyewe bila ushiriki wa binadamu, inayojulikana kwa kifupisho cha lugha ya Kiingereza kama M2M inakua Tanzania.

Teknolojia hii inawezesha vifaa kuwasiliana yenyewe na kubadilishana data na taarifa bila ushiriki wa binadamu.


Kati ya laini 86,847,460 zilizokuwepo Desemba, laini 85.8 milioni ni za mawasiliano kati ya watu na 1.01 milioni ni kwa mawasiliano ya mashine zenyewe bila kuingiliwa na binadamu.

Kuongezeka kwa laini za mashine kunaashiria kuenea Tanzania kwa teknolojia za kidijiti zinazojiendesha zenyewe. Laini za aina hii zilikuwa 962,928 Juni 2024.

**64.2%**

Hadi kufikia Desemba 2024 kulikuwa na laini za simu milioni 86.84 ikilinganishwa na milioni 52.88 za Machi 2021 sawa na **ongezeko la 64.2%.**

Kati ya zilizokuwepo Desemba 2024, laini **85.8 milioni** ni za mawasiliano kati ya watu (P2P) na **1.01 milioni** ni kwa mawasiliano ya mashine zenyewe bila kuingiliwa na binadamu.




Mifano ya teknolojia hiyo ni mita za kisasa za umeme na matumizi ya nishati, kamera za usalama wa maeneo ambavyo vinaweza kutuma taarifa kwenye simu ya mkononi ya mmiliki akiwa mbali.

Hii inamwezesha kufuatilia matumizi na matukio muda wote akiwa mbali.

Matumizi mengine ni kwenye mifumo wa usambazaji wa bidhaa ambapo majokofu ya kisasa yanaweza kuagiza vitu kwenye maduka kadri vinavyopungua.

Teknolojia pia inatumiwa kwenye vifaa vinavyovaliwa na wahusika, mithili ya saa za mkononi, ili kufuatilia afya, ukakamavu na shughuli za kila siku za mhusika.

Taarifa ya TCRA zinaonesha kwamba vifaa vya kuvaa mwilini 8,474 vilikuwa vimeunganishwa mitandaoni Tanzania Desemba 2024.

## Mwelekeo wa intaneti na masafa ya kasi

Eneo jingine lililokua kwa kasi na huduma kuenea zaidi miongoni mwa watu ni matumizi intaneti. Laini zilizotumiwa kwa huduma za intaneti zimeongezeka kutoka 29,071,817 Machi 2021 hadi 48,028,227 Disemba 2024.

Teknolojia za mawasiliano ya simu za mkononi zinazowezesha intaneti ya kasi zinazidi kuenea Tanzania, ikiwa ni pamoja na asilimia ya simu janja kwa idadi ya watu kuongezeka kwa pointi 11 ndani ya miaka minne.

Simu janja zimeenea kwa asilimia 36 miongoni mwa watu mwishoni mwa Desemba, kutoka asilimia 25 mwaka 2021.

Simu hizi zina uwezo mkubwa wa kikompyuta na zinawezesha kupakia na kupakua data, picha na video kwa kasi. Zinaendeleza matumizi ya intaneti. Takwimu za mawasiliano za Desemba 2024 zinaonesha kuwa wastani wa asilimia 99.8 ya watumiaji wa intaneti wanapata huduma hizo kupitia simu na vifaa vya mkononi, vikiwemo vishkwambi.

Matumizi ya data yanaongezeka Tanzania. Kiwango cha matumizi ya data kiliongezeka kwa asilimia 34, kutoka gigabaiti (GB) 766 milioni mwaka 2022 hadi bilioni 1.03 mwaka 2023.


Pamoja na simu janja, vifaa vingine vinavyowezesha matumizi ya intaneti pia .yameongezeka. Hivi ni pamoja na modemu, ambazo zimeenea kwa watu kwa asilimia 1.02.

## Huduma za pesa kwa simu

Akaunti za pesa kwa simu za mkononi zimeongezeka karibu mara mbili (asilimia) kati ya 2021 na Desemba 2024. Zilikuwa 61,882,499 Desemba 2024, kutoka 32,720,180.

Kiwango cha kuongezeka usajili wa akaunti za pesa kwa simu za mkononi kilizidi cha usajili wa laini za simu kati ya Desemba 2021 na Desemba 2024.

Hii inaonesha kwamba watumiaji wengi wa simu za mkononi wanajisajili kwa huduma za fedha mtandaoni na kidijiti, hivyo kuingia kwenye mfumo shirikishi wa kifedha.




*Ramani ya mkongo wa taifa wa mawasiliano ya kasi*

Wakati laini za simu zilizosajiliwa ziliongezeka kwa asilimia 65.4 kati ya Machi 2021 na Desemba 2024, akaunti za fedha kwa simu ziliongezeka kwa wastani wa asilimia 89.1.

Huduma za kifedha kupitia simu za mkononi zimeleta ufanisi kwa watumiaji na pia zimepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za uendeshaji kwa taasisi. Vilevile malipo ya kielektroniki yanawezesha mamlaka zinazosimamia mapato kudhibiti mapato ya serikali na sekta ya umma, hasa baada ya serikali kuanzisha mfumo wa malipo ya kiserikali mtandaoni (GePG).

TCRA inatoa leseni kwa watoa huduma za simu za mkononi na kuwapa namba za mawasiliano na misimbo, au namba fupi ya kuwezesha miamala hiyo.

Benki Kuu ya Tanzania inasimamia sekta ya fedha kwa ujumla na inatoa leseni za huduma za fedha mitandaoni. Taasisi hizi zinashirikiana kwenye masuala ya fedha mtandaoni.




| Desemba 2021 | 93.2% | Desemba 2024 |
| --- | --- | --- |
| Milioni 32.72 | | Milioni 63.21 |

**Faida**

- Huduma za fedha kupitia simu za mkononi zimeleta ufanisi kwa watumiaji na pia zimepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za uendeshaji kwa taasisi.
- Malipo ya kielektroniki yanawezesha mamlaka zinazosimamia mapato kudhibiti mapato ya Serikali na Sekta ya umma.
- Zimezalisha ajira nyingi, zikiwemo za uwakala.
- Zimepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za uendeshaji kwa taasisi, hasa baada ya Serikali kuanzisha mfumo wa malipo ya kiserikali mtandaoni (GePG).

## Kuongeza matumizi ya masafa ya kasi

Serikali imeainisha hatua inazochukua kueneza huduma za intaneti ya kasi na yenye ufanisi sehemu nyingi nchini. JUlai mwaka huu TCRA itatoa kwa njia ya mnada masafa kwenye bendi ya 3600 hadi 3800 MHZ.

Wachambuzi wameelezea mpango huo kuwa ni hatua ya kiusimamizi itakayochangia kuharakisha ajenda ya uchumi wa kidijitali Tanzania. Mnada huo utahusisha vitalu vinne vya masafa katika bendi hiyo, na ambayo yanavutia zaidi watoa huduma kwa kasi yake na ufanisi wake.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt Jabiri Bakari ameeleza kuwa matumizi ya masafa hayo yataongeza wigo wa utoaji huduma za kidijiti katika maeneo nchini. Yatawezesha yafuatayo:

- i. Kuendeleza miundombinu ya mawasiliano ya simu na intaneti ya kasi ambayo itachochea maendeleo ya uchumi wa Tanzania.
- ii. Ukuaji wa sekta nyingine.
- iii. Kuwezeshaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi kwenye utoaji wa huduma kama vile elimu, afya, kilimo, biashara, huduma za kifedha kupitia teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).
- iv. Kuimarisha ubora wa huduma za mawasiliano kwa watumiaji na kupanua utoaji wa huduma za mawasiliano ya simu na intaneti kwa Watanzania wengi zaidi
- v. Kukuza, kuimarisha na kuwezesha ubunifu wa huduma mpya za TEHAMA na matumizi yake.

Ili kuhakikisha kuwa watumiaji wananufaika kikamilifu na huduma za simu na intaneti, TCRA itaweka masharti ya usambazali na utoaji wa huduma kwa matumizi ya masafa husika.

Mnada wa masafa wa Julai mwaka huu utakuwa wa tatu kufanywa na TCRA, na wa pili kuendeshwa na wataalamu wake bila ushiriki wa mshauri mwelekezi. Oktoba 2022 TCRA iliuza kwa mnada vitalu 11 vya masafa kwenye bendi ya megahezi (Mhz) 700z Mhz 2300, Mhz 2600 na Mhz 3500.

Mnada huo, ambao ulipangwa na kusimamiwa na timu ya ndani ya TCRA, ulikuwa wa viwango vinavyokubalika kimataifa, kuanzia mwanzo hadi hatua ya kuuza na kutoa masafa kwa walioshinda.



*Rais Dkt Samia Suluhu Hassan akihutubia kikao cha 76 cha Umoja wa Ma-taifa jijini New York, Septemba 23, 2021.*

## Kuongezeka ufanisi kwenye utoaji na matumizi ya huduma

Serikali imekuwa inasisitiza umuhimu wa kutoa huduma za mawasiliano kwa gharama nafuu. Serikali inahimiza mipango inayobuni na kutekeleza mikakati ya kuweka mazingira bora ya ushindani na udhibiti katika sekta ya mawasiliano ili wananchi wengi zaidi wamudu gharama za mawasiliano.

Kukua kwa huduma za simu za mkononi kumewezesha kukua kwa huduma tegemezi, ambazo zimewapa wananchi uhuru zaidi wa kuwasiliana na kufanya miamala mbalimbali.

Fursa zinazowezesha wananchi kuendesha maisha yao kwa ufanisi kupitia huduma na teknolojia mpya zimeongezeka kwa kasi ndani ya miaka ya hivi karibuni.

Takwimu za TCRA zinaonesha kwamba wananchi wana uhuru zaidi wa kuchagua huduma na kukamilisha miamala kwa gharama nafuu.

Dr Bakari anaeleza kuwa kushuka huku kumechangiwa na kushuka kwa gharama za kuunganisha simu kati ya mitandao kwa dakika; kutoka shilingi 15.6 mwaka 2018 mpaka shilingi 1.68 Januari 2025.

## Kuimarika ushindani

Vichocheo vikuu vya ukuaji huu wa sekta ndani ya kipindi kinachochambuliwa ni matokeo ya kuongezeka miundombinu ya huduma na na usimamizi unaotegemewa na kutabirika.

Vilevile, ukuaji umechangiwa na ushindani kwenye sekta, hasa ya mawasiliano ya simu, ambao umewezesha kuenea kwa huduma, kupatikana kwake na kuchukuliwa kwa matumizi kwa wingi zaidi.

**Ushindani umekuwa na sura mbili...**

1. **Kama kichocheo cha ukuaji.**
2. **Kama matokeo ya hatua madhubuti za kiusimamizi.**

Watoa huduma sasa wanashindana kwenye kuboresha huduma na kuridhisha wateja wao, ikiwa ni pamoja na ubunifu na kuanzisha huduma za ziada.

## Huduma za Sekta ya Utangazaji

Takwimu za utangazaji zinaonesha kuwa visimbuzi milioni 2.13 viko hewani mpaka kufikia mwezi Desemba 2024 ikilinganishwa na visimbuzi milioni 2.81 mwezi Machi 2021 ikiwa ni pungufu ya asilimia 22.78. Kati ya hivyo, 580,522 ni vya kidijiti kwa mfumo wa televisheni wa utangazaji wa mitambo ya ardhini (DTT) na 1,568,241 ni vya mfumo wa televisheni wa satelaiti (DTH).

Kwa upande wa huduma za Utangazaji wa redio, takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 78.7 ya watu wanafikiwa na huduma za Utangazaji wa FM ambalo ni ongezeko la asilimia 6.9.

TCRA na wadau wa maudhui wanajitahidi kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa maudhui stahiki kupitia mitandao yanayokidhi mahitaji ya wananchi kiutamaduni, kijamii na kuwezesha kujiendeleza kiuchumi.

Pamoja na kuenea huduma za utangazaji, Tanzania imejipanga kutekeleza mambo mapya matatu kuhakikisha matangazo yanafikia wasikilizaji na watazamaji wengi zaidi, na pia kuboresha ubora huduma za maudhui.

Tanzania ilipata nafasi anga za juu kwa ajili ya mzunguko wa setilaiti yake ya kwanza ya mawasiliano. Mafanikio haya yalipatikana kwenye Mkutano wa Kimataifa wa Mawasiliano ya Redio, uliofanyika Dubai, Falme za Kiarabu mwaka 2023.

Vilevile miundombinu ya utangazaji inawekwa maeneo yenye ugumu kufika mawimbi ya redio na televisheni, na ambayo kwa wawekezaji hayana 'mvuto' kibiashara na hivyo kutokufikiwa na huduma ipasavyo. Mfuko wa UCSAF unatekeleza miradi hii.

TCRA imeainisha maeneo yenye huduma hafifu na yasiyo na huduma za mawasiliano ya simu na intaneti baada ya kufanya utafiti nchini kote. Imewasilisha taarifa ya utafiti huo kwa huduma ili waboreshe huduma kwenye maeneo hayo.

TCRA inasimamia utangazaji Tanzania Bara, na inayo kamati mahsusi inayoshughulikia maudhui. Kamati hiyo inafuatilia uzingatiaji maadili na kanuni za maudhui ya redio, televisheni na mtandaoni kwa wenye leseni ya Mamlaka.

TCRA inashirikiana na Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari kwenye kuendeleza maadili na weledi kwenye uaandaji na utoaji maudhui.

Bodi hiyo ilizinduliwa 3 Machi mwaka huu. Inatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika kuhakikisha sekta ya utangazaji inazingatia maadili, kanuni na weledi katika utendaji kazi wake.

## Posta na usafirishaji vifurushi

Tanzania ina mipango ya kujiimarisha kama kitovu cha mawasiliano ya posta Afrika. Tanzania, ambayo imezungukwa na nchi nane – kati ya hizo tano zikiwa hazina mwambao wa bahari – iko kwenye nafasi ya kimkakati ya kufaidi matunda ya biashara mtandao miongoni mwa nchi za Afrika.

Hii inaweza kuwa moja kwa moja au kupitia shughuli kwenye hatua mba-limbali za utoaji huduma za posta

Tanzania imeweka miundombinu muhimu ya huduma za posta zinazowezeshwa na ub-nifu, ikiwa ni pamoja na mfumo wa anwani za makazi na postikodi ambao unawezesha ufikishaji na uchukuaji vitu vinavyonunuliwa mitandaoni na kuhitajika kufikishwa kwenye makazi au ofisi za wahusika.

Mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali inatekeleza mradi wa kujenga kituo cha kikanda kitakachojumuisha



maghala maalum ya kuhifadhi bidhaa, huduma ya ugomboaji na ushuru wa forodha ili kuwezesha biashara mtandao. Tanzania ina nafasi kubwa ya kuwa kinara wa biashara mtandao Afrika. Imezungukwa na nchi nane – kati ya hizo tano ziki-wa hazina mwambao wa bahari. Hii inaweza kuwa moja kwa moja au kupitia shughuli kwenye hatua mbalimbali za utoaji huduma za posta.

Vilevile Tanzania inaimarisha shughuli za usafirishaji mizigo kwa ndege. Shirika la ndege Tanzania– Air Tanzania – lina ndege kubwa ya mizigo ambayo inaweza kusafirisha mizigo ndani ya Afrika na sehemu nyingine ulimwenguni. Ufanisi wa usafirishaji mizigo utaiweka Tanzania kwenye nafasi kubwa ya kunufaika na ukuaji biashara mtandao Afrika, Tanzania na shirika lake la ndege.

Shirika la ndege Tanzania – Air Tanzania – lina ndege kubwa ya mizigo ambayo inaweza kusafirisha mizigo ndani ya Afrika na sehemu nyingine ulimwenguni. Ufanisi wa usafirishaji mizigo utaiweka Tanzania kwenye nafasi kubwa ya kunufaika na ukuaji biashara mtandao Afrika. Tanzania na shirika lake la ndege.

Katika kipindi cha Machi 2021 hadi Desemba 2024 kumekuwa na ongezeko la watoa huduma za Posta na Usafirishaji wa Vifurushi na Vipeto kutoka 119, Machi 2021 hadi kufikia 148, Desemba 2024, na tano (5) za programu tumizi maalum kwa biashara mtandao.

Leseni ya programu tumizi kwa ajili ya biashara mtandao inafuatia marekebisho ya kanuni za leseni mwaka 2022.

Mwaka wa fedha 2024/25 Serikali imepanga kuwezesha Mfumo wa Anwani za Makazi (NaPA) kuunganishwa na mifumo mingine ya kutolea huduma za kijamii; Mfumo huu unafanikisha shughuli za taasisi za dola, unainua ubora wa huduma za kusambaza barua, vifurushi na vipeto nchini na kimataifa kati ya Tanzania na nchi nyingine.

Vilevile umewezesha kuanzishwa kanzidata inayoweza kutumiwa na wafanyabiashara kama nyenzo muhimu ya kutangaza biashara zao na kwa tafiti za takwimu.



## Tanzania inavyoondoa tofauti matumizi ya TEHAMA

Ripoti nyingine ya EACO inaonesha kuwa Tanzania imefikia hatua muhimu kwenye juhudi zake za kuondoa tofauti kwenye maeneo ya TEHAMA wezeshi na muhimu.

Tanzania imepunguza tofauti katika kuenea kwa huduma za mawasiliano miongoni mwa watu, kijiografia na kwenye uwezo wa kumiliki na kutumia vifaa vya kielektroniki.

Tofauti za kwenye mawasiliano zinatokana na kutokuwa na usawa kwenye upatikanaji, kuchukuliwa kwa matumizi na kutumika teknolojia za habari na mawasiliano (TEHAMA) na huduma kati ya maeneo na miongoni mwa watu. Vilevile zinahusu kutokuwepo usawa kwenye uchukuaji kwa matumizi ndani ya maeneo na makundi ya watu.

Mipango inayosukuma kutumika TEHAMA na juhudi za pamoja zinazoleta tija zaidi mi-ongoni mwa wadau wa TEHAMA vinawezesha nchi kupunguza tofauti za mawasiliano kidijiti. Mipango thabiti ya kutumia kikamilifu raslimali adimu pia inachangia.

Durusi zinaonesha kuwa mipango ya kuweka miundombinu mipya peke yake haziwezi kuondoa tofauti za mawasiliano kidijiti. Inatakiwa itekelezwe sambamba na kuwezesha uchukuliwaji kwa matumizi na utumiaji wa huduma zinazowezeshwa na teknolojia zilizosimikwa.

**FAHAMU**

***Tanzania ina sera imara na mfumo makini wa usimamizi wenye mwelekeo sahihi. Imeboresha kuenea kwa TEHAMA miongoni mwa watu na maeneo mengi nchini.***

Ripoti ya Benki ya Dunia kuhusu namna Mabadiliko ya kidijitali yanavyoongeza kasi ya maendeleo Afrika, inaeleza kuwa mafanikio ya Tanzania yametokana na ujenzi wa miundombinu wezeshi, sera nzuri na mfumo imara wa usimamizi.

Ripoti ya Benki ya Dunia kuhusu namna Mabadiliko ya kidijitali yanavyoongeza kasi ya maendeleo Afrika, inaeleza kuwa mafanikio ya Tanzania yametokana na ujenzi wa miundombinu wezeshi, sera nzuri na mfumo imara wa usimamizi.


Inataja sheria nzuri na kuimarishwa kwa mifumo utoaji leseni kama viwezeshi vingine vya mafanikio haya.

Msimamizi wa sekta – TCRA, imeendelea kujiimarisha kwa kuwezesha mazingira bora na yenye ufanisi ya uwekaji wa miundombinu ya utoaji huduma.

Ufuatiliaji wa masharti ya leseni zinazotolewa kwa huduma mbalimbali umeongeza ufanisi na ubora wa huduma. Yote haya ni sehemu ya kubuni na kutekeleza mikakati ya kuweka mazingira bora ya ushindani na udhibiti katika sekta ya mawasiliano ili wananchi wengi zaidi wamudu gharama za mawasiliano.

## Tanzania yajiimarisha kimataifa sekta ya mawasiliano

Tanzania imeendelea kutoa mchango wake kimataifa kwenye taasisi za mawasiliano. Ni mwenyeji wa Umoja wa Posta Afrika (PAPU) – makao yako Arusha. Tanzania pia ni mjumbe wa kwenye Mabaraza ya utendaji ya taasisi nyingi za mawasiliano ulimwenguni.



Taasisi hizo ni pamoja na PAPU, Umoja wa Posta Ulimwenguni (UPU), Umoja wa Mawasiliano Afrika (ATU), Shirika la Mawasiliano Ulimwenguni (ITU) na Umojs wa Mawasiliano ya Simu Jumuiya ya Madola (CTO).

Tanzania ni ya kwanza Afrika Mashariki, ya tatu Afrika kwa viwango vya juu vya usalama mitandaoni, kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa hivi karibuni na Shirika la Mawasiliano ya Simu Ulimwenguni (ITU).

Tanzania pia ni mojawapo ya nchi 46 duniani zinazoongoza kwa kuzingatia kanuni za usalama mitandaoni. Kipindi hiki kimeshuhudia kuanzishwa kwa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Hatua zinaendelea kuchukuliwa kuongeza faragha na usiri wa taarifa za wananchi katika mawasiliano kwa kukamilisha kutunga sheria ya kuimarisha ulinzi wa taarifa na takwimu.

Vilevile Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt Bakari ni mjumbe wa Bodi ya Wadau wa Usimamizi wa Bunifu ya ITU. Sambamba na hili, ITU imechagua Tanzania kuwa mojawapo ya nchi za Afrika zitakazokuwa na vituo vya msaada wa kiufundi kwa vituo vya ubunifu.

Kituo hicho cha kitaifa cha ubunifu katika teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kinakusudiwa kujenga uwezo, na kuchochea ubunifu wa kidijitali nchini. Dkt Bakari ameeleza kuwa kituo hicho kinalenga kuchochea mabadiliko ya ikolojia nzima ya ubunifu Tanzania.

Vile vile ITU imetoa ripoti hivi karibuni kuhusu Tanzania na usimamizi wa sekta ya mawasiliamo. Tanzania ina alama zaidi ya wastani wa Afrika kwenye nguzo zote za usimamizi shirikishi na viashirio vyake.

Mifano ya usimamizi shirikishi Tanzania ni kwenye sekta ya pesa kwa simu, usalama na ulinzi mitandaoni, matumizi ya masafa, na usafiri angani, majini na nchi kavu.

TCRA inashirikiana na Benki Kuu ya Tanzania kwenye masuala ya pesa kwa simu za mkononi, inafanya kazi na Mamlaka ya Usimamizi Usafiri wa Anga kwenye upangaji na matumizi ya masafa.

Vilevile watoa huduma wanatumia data za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA kwenye usajili wa laini za simu za mkononi.

Alama ya Tanzania kwa mwaka 2023 kwenye misingi ya muundo wa Sera katika eneo la kidijitali ilikuwa karibu mara mbili ya wastani kwa Afrika. Kiwango hicho ni juu ya wastani wa nchi za Afrika na kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

TCRA inaelekea vizuri kwenye aina mpya ya usimamizi wenye kiwango sanifu cha kimataifa. ITU imesema TCRA ina nyenzo zote muhimu kuelekea daraja la juu zaidi la usimamizi unaozingatia miongozo na kanuni imara kuliko utaratibu wa kawaida.




MAKALA MAALUM


# Tanzania yaimarisha uwezo, fursa biashara mtandao

Na Mwandishi wetu

Tanzania inaimarisha miundombinu wezeshi na mifumo muhimu ya kufikisha kwenye makazi ya watu bidhaa zinazonunuliwa kupitia mtandao. Tanzania ina miundombinu na programu wezeshi zinavyofanikisha intaneti ya kasi na mfumo wa malipo kidijiti, vijenzi muhimu vya biashara mtandao.

Hatua za kisera na kiusimamizi zinazotekelezwa Tanzania zimezingatia mambo yote yanayowezesha biashara mtandao. Hadi Desemba 2024 TCRA ilishatoa leseni za huduma wezeshi za mitandao. Hawa wanawezesha upatikanaji wa huduma za intaneti.

Watumiaji waliopata huduma za intaneti kupitia vifaa vya mkononi vilivyounganishwa kwa waya na visivyounganishwa waliongezeka kutoka 29,071,817 Machi 2021 hadi 48,028,227 Disemba 2024.




Aidha, akaunti za simu za mkononi, ambazo zinawezesha malipo mtandaoni zilifikia 60,815,533 ambazo zilifanya miamala 310,881,561 Septemba mwaka huu, Dkt Bakari aliongeza.

Biashara mtandao pia inategemea mifumo imara ya usafiri na usambazaji. Urahisi wa kufikisha majumbani au maofisini vifaa vinavyoagizwa kidijiti unatokana na kukua kwa mawasiliano ya mkononi, matumizi ya intaneti, mitandao ya kijamii, fursa za kutangaza na biashara mitandaoni na ufanisi wa mawasiliano.

Serikali inasimamia mipango ya kuendeleza biashara mtandao. Inaunganisha mfumo wa taifa wa anwani na postikodi (NAPS) na mifumo mingine na majukwaa ya huduma za kijamii.

> **"*Serikali imechukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa anuani za makazi zinawekwa nchini ili kurahisisha upatikanaji, utoaji na ufikishishaji wa huduma mbalimbali.***

Vilevile imeanzisha mpango wa kujenga maghala la kuhifadhi vitu vinavyoingia Tanzania kwa mfumo wa biashara mtandao.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt Bakari alieleza kuwa NAPS imebadilisha utoaji wa huduma za kiposta na usafirishaji wa vifurushi Tanzania. Vifaa vinavyonunuliwa kielektroniki vinafikishwa kwa wateja kupitia anwani zi-nazofahamika.

Ufikishaji huu unafanywa na watoa huduma za usafirishaji vifurushi, au kwa utaratibu mwingine unaohusisha magari madogo na pikipiki zinazobeba abiria (bodaboda).

Pamoja na kuwezesha utoaji wa huduma, NAPS inafanikisha shughuli za kiserikali na uendeshaji. Mfumo unafanikisha mawasiliano ya serikali na wananchi.

Mfumo huu, unaoratibiwa na TCRA, ulifanikisha sana sensa ya watu na makazi 2022. Hii ilikuwa baada ya Rais wa Awamu ya Sita, Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan kutoa maelekezo mahsusi ya kuuimarisha.


KUTOKA MAKTABA

# Agenda kuidijiti Tanzania

***Sehemu ya hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, alipolihutubia Bunge la 12 la Jamhuri Ya Muungano wa Tanzania Dodoma, 22 Aprili 2021.***

Mheshimiwa Spika; mbali na miundombinu migumu, tutaimarisha pia miundombinu laini, hususan miundombinu ya teknolojia ya mawasiliano.

Kama inavyofahamika, dunia ipo kwenye Mapinduzi ya Nne ya Viwanda, ambayo yanaongozwa na sekta ya Teknolojia ya Mawasiliano (TEHAMA), na kwa maana hiyo, uchumi wa dunia pamoja na shughuli nyingi duniani, kwa sasa, zinafanyika kwa kutumia TEHAMA.





Hivyo basi, sisi Tanzania nasi hatuna budi kuweka mkazo mkubwa katika kukuza sekta hii.

Kwa msingi huo, tumepanga, kwenye miaka hii mitano, pamoja na masuala mengine, kuongeza kasi ya kufikisha miundombinu ya Mkongo wa Taifa kwenye maeneo mengi ya nchi yetu, hususan katika ngazi za Wilaya, na pia kuongeza wigo wa matumizi ya mawasiliano ya kasi (yaani broadband) kutoka asilimia 45 ya sasa hadi asilimia 80 ifikapo mwaka 2025.

Aidha, kuongeza watumiaji wa intaneti kutoka asilimia 43 ya sasa hadi asimilia 80 mwaka 2025; na pia, kuboresha upatikanaji wa mawasiliano ya simu nchi nzima.

Tutatoa kipaumbele kwenye masuala ya utafiti na ubunifu kwenye TEHAMA pamoja na kuimarisha usalama kwenye masuala ya Mawasiliano.

DONDOO

# Ilani ya CCM Uchaguzi Mkuu 2020 na Sekta ya mawasiliano

Na Mwandishi wetu

Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi wa Rais, Dkt Samia Suluhu Hassan inatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020 ya Chama Tawala.

Vifungu 61; 102; 103 na 125 vinazungumzia maeneo ambayo yanasimamiwa na TCRA. Hayo ni pamoja na kueneza huduma za simu, intaneti na utangazaji.

## Baadhi ya malengo kwenye Ilani ni:

1. Kuongeza faragha na usiri wa taarifa za wananchi katika mawasiliano kwa kukamilisha kutunga sheria ya kuimarisha ulinzi wa taarifa na takwimu. Sheria ya Ulinzi wa taarifa binafsi imetungwa na inatumika. Vilevile, faragha na usiri wa watumiaji vinalindwa na Kanuni mbalimbali zilizotungwa chini ya Sheria ya Mwasiliano ya Kielektroniki na Posta (EPOCA) na ambazo zinaboreshwa mara kwa mara.

2. Kuimarisha mfumo wa TEHAMA wa kudhibiti usalama na mapato katika mawasiliano.

3. Kuimarisha mtambo wa kusimamia mawasiliano wa TTMS ili kuhakikisha upatikanaji wa mapato stahiki kwa malipo ya kodi na kuboresha mawasiliano na udhibiti wa matumizi ya mawasiliano.TCRA inaendesha mtambo wenye mfumo wa kusimamia mawasiliano ya simu (TTMS). Mfumo huo unatambua mapato na takwimu za miamala ya fedha mitandaoni. Vilevile una kanzidata ya laini za simu za mkononi na namba tambulishi ya vifaa vya mawasiliano.


4. Kuongeza mchango wa sekta ya mawasiliano kwenye Pato la Taifa kwa kuongeza matumizi ya TEHAMA. Matumizi ya TEHAMA kwenye maeneo mbalimbali yameongezeka kwa hadi asilimia 89 kwenye baadhi ya huduma kati ya Machi 2021 na Desemba 2024.

5. Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuweka mazingira bora ya ushindani na udhibiti katika sekta ya mawasiliano ili wananchi wengi zaidi wamudu gharama za mawasiliano. Wingi wa leseni zilizotolewa na kushuka kwa gharama za huduma ni mojawapo ya matokeo ya ushindani.

6. Kuongeza wigo na matumizi ya mawasiliano ya kasi.

7. Kuongeza watumiaji wa intaneti. Wameongezeka kwa asilimia 65; kutoka 29,071,663 Machi 2021 mpaka 48,028,227 Desemba 2024.

8. Kuboresha huduma za mawasiliano ya simu za viganjani ili kupatikana maeneo yote. Laini zimeongezeka kwa asilimia 67; kutoka 53,813,930 mpaka 87,448,346 kipindi hicho. Akaunti za pesa kwa simu ziliongezeka kwa asilimia 89; kutoka 32,720,180 mpaka 61,882,499.



**9** Kuweka mazingira wezeshi ya kuanzisha viwanda vya uzalishaji wa vifaa vya TEHAMA vyenye uwezo wa kutoa ajira kwa wananchi waliowengi na kuzalisha vifaa vinavyotumika ndani na nje ya nchi, na kujenga kiwanda cha kuchakata taka za kielektoniki ili kudhibiti uharibifu wa mazingira. Tanzania imechukua hatua kuzuia uingizwaji nchini vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki vyenye viashiria vya kuwa ni taka ili kuzuia nchi isiwe jalala ya vifaa vya kielektroniki vilivyotumika.

Hatua za kisheria na kiusimamizi ni pamoja na kutoza ada ya uchakavu wa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki vinavyoingizwa nchini. Vifaa vinavyoelekea Tanzania vinakaguliwa kule vinakotoka na kutozwa ushuru unaoitwa tozo ya mazingira, ambao utachangia gharama za kuvitekeketeza baada ya kumalizika muda wa matumizi.

**10** Kuhamasisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kutoa huduma, biashara na uzalishaji ili kuongeza uwazi, ufanisi, na kuboresha maisha ya wananchi kichumi na kijamii.

**11** Kuhakikisha anuani za makazi zinawekwa nchini ili kurahisisha upatikanaji, utoaji na ufikishishaji wa huduma mbalimbali.

**12** Kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa maudhui stahiki yanayokidhi mahitaji ya wananchi kiutamaduni, kijamii na kuwawe zesha kujiendeleza kiuchumi. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaratibu programu maalumu ya kuandaa vipindi vya maadili vitakavyorushwa na vituo vya utangazaji vyenye leseni ya kiwilaya ili kujenga nchini jamii yenye maadili mema.

Chini ya mpango huo; unaotekelezwa kwa ushirikiano na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalum; vituo 14 vyenye leseni ya Kitaifa vinarusha vipindi vinavyotoa elimu ya malezi bora ya familia na vijana.

Lengo ni kuimarisha utoaji elimu na kujenga jamii inayozingatia maadili, mila desturi na utamaduni wa Mtanzania, ameeleza na kuongeza kuwa mpango huo pia utahusisha kuandaa na kutoa katuni za watoto na ngoma za asili. Mpango wa uandaaji wa ngoma za asili umeshirikisha Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na Chuo Kikuu cha Dodoma.

Hatua hizi zimechuku¬liwa kama sehemu ya jitihada za kupambana na maudhui yanayotoka nje ya nchi ikiwa ni pamoja na katuni za watoto zisizo na maadili ya Kitanzania.

TCRA inahimiza utengenezaji, uzalishaji na usambazaji wa maudhui ya ndani. TCRA imeshafanya vikao vingi na watengenezaji maudhui wanaojitegemea kujadili namna ya kuboresha kazi zao.



**13** Kuimarisha mfumo wa uratibu wa shughuli za sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchangia kikamilifu katika ujenzi wa uchu mi imara na endelevu;

**14** Kuimarisha na kuhamasisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika uchumi wa kidijitali (digital economy) husu san Serikali mtandao, miundombinu ya TEHAMA katika Nyanja zote za uchumi na ulinzi wa mitandao;

**15** Kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuendeleza na kuongeza uwezo wa kitaalam na matumizi ya teknolojia mpya za kidijitali;

**16** Kuhamasisha matumizi ya mitandao ya kijamii ili kuongeza upatikanaji wa habari. TCRA imetoa leseni 210 za maudhui ya tel- evisheni mtandaoni, 10 za redio mtandaoni na sita za kuandaa na kusambaza maudhui mtandaoni.

MAKALA MAALUM

# TCRA inavyojipambanua na mikakati ya kitaifa

Na Mwandishi wetu

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imesawanisha mipango yake na ile ya kitaifa, ikiwemo ile ya serikali, ambayo inatekeleza Ilani ya Chama Tawala.

TCRA inaweka na kusimamia mfumo wa usimamizi wa sekta ya mawasiliano kwa ufanisi kwa lengo la kuendeleza ushindani, uvumbuzi na upatikanaji wa fursa za kidijitali kwa wote.

Wajibu huu unahusisha pia kuchochea ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano ya simu maeneo ya pembezoni na kuhimiza mipango ya kujenga uelewa wa masuala ya kidijitali kwa wananchi na watumiaji.


TCRA inaweka mazingira wezeshi ya usimamizi, inahimiza mipango shirikishi na inashirikiana na wadau mbalimbali. TCRA pia inawezesha watoa huduma kupanua huduma zao nchini.

**TCRA inatarajia kufanya mnada wa masafa kwenye vitalu vinne**

**JULAI 2025**

**Bendi za masafa ya**

**3600 - 3800MHZ**




TCRA ina mipango kuongeza wigo wa masafa kwa watoa huduma. Julai mwaka huu itagawa, kwa mnada, vitalu vinne vya masafa kwenye bendi za 3600-3800.

Masafa hayo yanapendelewa zaidi kwenye utoaji wa huduma za mawasiliano ya simu na vifaa vya mkononi kwa kutumia teknolojia ya uzao wa tano (5G).



Teknolojia hii inatarajiwa kuwa mhimili mkubwa kwenye mkakati wa Tanzania wa kuweka misingi imara ya kujenga uchumi wa kidijiti.

Kipindi hiki na kijacho kitashuhudia mabadiliko na maendeleo ya kasi katika TEHAMA.

Teknolojia zinazoibuka ni pamoja na mifumo ya kompyuta inayoweza kufanya kazi ambazo kwa kawaida zinahitaji akili na utashi wa binadamu; matumizi ya maroboti na matumizi ya mifumo ya kompyuta kuonesha hali halisi ya maisha.

Nyingine ni matumizi ya seti kubwa za data zinazoweza kuchambuliwa ili kuonyesha mwelekeo, hasa kuhusiana na vitendo vya binadamu.

Vilevile kuna teknolojia za mambo yanayowezesha maumizi ya data kuboresha uwezo wa kompyuta kufanya mambo mbalimbali na vitu kuwasiliano vyenyewe kupitia mfumo wa intaneti.

> TCRA imeandaa miongozo ya kusimamia teknolojia mpya. Kwa mfano, mpango wa namba wa kitaifa una namba kwa ajili ya mwasiliano ya mashine kwa mashine.

Mkakati mwingine muhimu unaotekelezwa na TCRA ni mpango wa kuwezesha kampuni zinazochipukia katika sekta ya teknolojia za kidijiti na wavumbuzi wanaobuni huduma mpya za mawasiliano.

TCRA inawapatia wavumbuzi hao raslimali muhimu za mawasiliano bila malipo na kwa vipindi maalum ili wajaribu miradi yao. Raslimaloi hizi ni pamoja na namba, misimbo, masafa, vikoa vya Tanzania na postikodi.

Hatua hii inalenga kuweka mazingira bora ya kuvutia uvumbuzi wa kidijiti nchini na kuhakikisha kuwa kampuni hizo zina nafasi ya kukua na kufanikiwa.

Mpango huo, unaolenga kuwapa wabunifu zana wanazohitaji kwa majaribio ya huduma zao kwa kipindi maalum, unatarajiwa kuendeleza na kubadili mazingira ya TEHAMA Tanzania.

TCRA pia inasimamia mpango wa uanzishwaji na uratibu wa klabu za masuala ya kidijiti katika shule, vyuo na vyuo vikuu nchini.

Klabu hizi ni majukwaa ya hiari yanayowakutanisha wanafunzi wa rika moja kupata uelewa na kuhamasishana juu ya TEHAMA, uchumi wa kidijiti na fursa zake. Ni sehemu ya mkakati wa kujenga Tanzania ya kidijiti.

Dkt Bakari ametaja faida za klabu hizo kuwa ni kupunguza pengo la ujuzi wa kidijiti, kuongeza stadi za Kidijiti miongovijana, kuongeza na kukuza ajira na kuhamasisha ubunifu kwa wanafunzi. Vilevile zinawajengea vijana fikra zenye mantiki, na kutatua changamoto zinazowakabili.


Vilevile klabu hizi zitachangia kupanua uelewa masuala ya TEHAMA na uchumi wa kidijitali, vitatoa fursa za kuendeleza stadi katika TEHAMA na zitawezesha kuimarika kwa matumizi ya mifumo ya kidijitali Tanzania.



# Sekta ya Mawasiliano katika namba

## Kuenea kwa teknolojia za mawasiliano ya simu na intaneti

**Mwenendo wa kuenea kwa uzao wa simu za mkononi miongoni mwa watu Tanzania kati ya 2021 na 2024 (Asilimia)**




**20%**

Uzao wa tano (5G) unaowezesha intaneti ya kasi kubwa umeenea kwa asilimia 20 ya watu na umeanza katika kipindi hiki cha miaka minne.

**88%**


Asilimia ya watu waliofikiwa na intaneti ya kasi ya 3G imefikia 91 na 4G imefikia 88 ambayo imepita lengo la Serikali la asilimia 80 kufikia 2025.

## Laini za huduma ya intaneti zaongezeka

Laini zinazotumiwa kwa huduma za intaneti zimeongezeka kwa 65.2%

| Machi 2021 | 65.8% | Disemba 2024 |
|---|---|---|
| Milioni **29.07** | | Milioni **48.02** |

Ongezeka hilo limechangiwa na uboreshaji wa miundombinu ya mawasiliano na ongezeko la matumizi ya simu janja.



## Huduma za Posta na Usafirishaji wa Vifurushi na Vipeto zaendelea kuimarika

Watoa huduma za Posta na Usafirishaji wa Vifurushi na Vipeto wameongezeka kwa 24.3% kutoka **119**, Machi 2021 hadi kufikia **153**, Desemba 2024.


Watoa huduma wengine 5 wanaotumia programu tumizi maalum kwa biashara mtandao wamesajiliwa katika kipindi hicho.

**5**

Mafanikio hayo yamechangiwa na Serikali kuweka miundombinu muhimu ya huduma za posta zinazowezeshwa na ubunifu, ikiwa ni pamoja na mfumo wa anwani za makazi na postikodi ambao unawezesha ufikishaji na uchukuaji vitu vinavyonunuliwa mitandaoni na kuhitajika kufikishwa kwenye makazi au ofisi za wahusika.


# Huduma sekta za utangazaji nazo kileleni

## Visimbuzi milioni 2.13



Visimbuzi **milioni 2.13** viko hewani mpaka kufikia mwezi Desemba 2024 ikilinganishwa na visimbuzi **milioni 2.81** mwezi Machi 2021 ikiwa ni pungufu ya **asilimia 22.78**.

## Kati ya visimbuzi hivyo...






**78.7% ya watu**


Tanzania wanafikiwa na huduma za utangazaji wa FM ambalo ni ongezeko la asilimia **7** ndani ya kipindi cha miaka 4 ya uongozi wa Rais Dk Samia Suluhu Hassan.

## Maudhui ya ndani, maudhui rafiki



TCRA na wadau wa maudhui wanajitahidi kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa maudhui stahiki kupitia mitandao yanayokidhi mahitaji ya wananchi kiutamaduni, kijamii na kuwezesha kujiendeleza kiuchumi.

### Mwenendo wa Ving'amuzi vilivyounganishwa kwa huduma za televisheni mfumo wa ardhini (DTT) na mfumo wa setilaiti (DTH)






**16,767**

Wateja walioungenishwa na huduma za televisheni kwa waya hadi Disemba 2024

KAMPENI

# Wadau waimarisha uthibiti ulaghai mitandaoni

Na Mwandishi wetu

Serikali imejipanga kukabiliana na uhalifu kwenye mitandao ya simu za mkononi na intaneti na imewakumbusha watumiaji wa huduma za mawasiliano kuzingatia tahadhari na elimu inayotolewa kuhusu matumizi sahihi na salama ya mitandao.

Waziri wa Mawasilino na Teknolojia ya Habari, Mhe. Jerry Silaa (Mb.) amesema Usalama wa Mitandao ya simu za mkononi utajenga imani ya wananchi, utawalinda watumiaji na kuendeleza shughuli mbalimbali za uchumi wa kidijiti zinazotegemea mitandao salama.

Mhe. Silaa alikuwa akizindua awamu ya pili ya kampeni inayoitwa "Sitapeliki" ambayo inahamasisha wananchi na watumiaji kuhusu njia za kuwa salama mitandaoni na kuepuka ulaghai.

Kampeni hiyo inaendeshwa kwa pamoja na watoa huduma, na wadau wengine wakiongozwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Ni njia mojawapo ya kukabiliana na matukio ya uhalifu kwenye mitandao ya simu za mkononi.

Mhe. Silaa alieleza kuwa huduma za mawasiliano Tanzania zimeenea sana na zinachangia ukuaji wa uchumi wa kidijiti na ustawi wa wananchi.

> ***"Serikali haitavumilia wachache wanaotaka kuleta hofu na kuondoa imani ya matumizi ya huduma za kidijiti - Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa.***

Kampeni ya SITAPELIKI inafuatia maazimio ya mkutano uliofanyika tarehe 22 Novemba 2024 ulioshiriki-sha Mawaziri, Makatibu Wakuu, Watendaji wa Serikali na Taasisi za Umma na Watoa Huduma kuhusu mbinu za kukabiliana na kadhia ya ulaghai kwenye mitandao ya simu za mkononi na intaneti.



*Meneja wa TCRA Kanda ya Ziwa Mhandisi Imelda Salum akitoa mada kwenye mojawapo ya kampeni za elimu kuhusu matumizi salama ya mitandao.*

Mhe Silaa amesisitiza kuwa Usalama na uimara wa mitandao unaongeza imani ta watumiaji na kuchangia kukua kwa huduma za kifedha kupitia simu za mkononi.

Amesema ulaghai mitandaoni unahujumu mikakati ya serikali kuendeleza ushirikishaji wa wananchi kwenye mifumo ya kifedha na kujenga uchumi wa kidijiti.

"Akaunti za pesa kupitia simu za mkononi zinawawezesha watu wengi zaidi kuingia kwenye mfumo shirikishi wa kifedha".

Ndani ya miaka mitano ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Tawala, tumeshuhudia akaunti za pesa kwa simu za mkononi zikiongezeka kwa asilimia 139, kutoka 26,503,777 mwaka 2020 hadi 63,207,569 Desemba 2024," amesema.

Ameeleza kuwa huduma za fedha kupitia simu za mkononi zimeleta ufanisi kwa watumiaji na pia zimepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za uendeshaji kwa taasisi.



Vilevile malipo ya kielektroniki yanawezesha mamlaka zinazosimamia mapato kudhibiti mapato ya Serikali, sekta ya Umma na binafsi.

Ulaghai hufanyika kwa matapeli hupiga simu na kutuma ujumbe mfupi, yaani meseji za ulaghai kwa watumiaji na kuwataka watoe taarifa zinazohusu akaunti zao za pesa kwa simu au za kibenki, miamala, nywila na namba za siri. Hii inawawezesha wahalifu hao kuiba kwenye akaunti za pesa kwa simu, benki au za wakala wa huduma za pesa mtandao.

Utapeli mwingine ni kulaghai watumiaji wa intaneti kubofya viunganishi (link) vilivyowekwa na matapeli wa mitandaoni, kujibu ujumbe wa barua pepe unaohusiana na fursa za kupata pesa za bure na matokeo yake taarifa za mhusika kuibiwa na matapeli.

Awamu ya pili ya kampeni ya elimu kwa umma inaendeshwa chini ya kaulimbiu ya "SITAPELIKI". Inaendeshwa kwa pamoja na watoa huduma, na wadau wengine wakiongozwa na Mamlaka ya mawasiliano Tanzania (TCRA). Hii ni moja ya njia za kukabiliana na matukio ya uhalifu kwenye mitandao ya simu za mkononi.

Mhe. Silaa amesisitiza kuwa serikali imejipanga kukabiliana na uhalifu kwenye mitandao ya simu na intaneti.

Matukio ya ulaghai kupitia simu za mkononi Tanzania yamepungua kwa asilimia 19 kati ya Septemba na Desemba mwaka jana, ingawaje yameongezeka kiuwiano mikoa ya Rukwa na Morogoro.

Taarifa ya ulaghai mitandaoni iliyotolewa hivi karibuni jijini Arusha kwenye uzinduzi wa awamu ya pili ya kampeni ya usalama mitandaoni inaonesha Rukwa ilikuwa na matukio 5,305 kati ya 12,896 nchi nzima Desemba 2024 huku Morogoro ikiwa na 4,278.

Uchambuzi unaonesha kuwa ingawaje matukio yamepungua Rukwa kutoka 5,571 Septemba mwaka jana, mkoa huo una asilimia 41 ya matukio yote nchini.

TCRA na Watoa Huduma wameandaa ujumbe kwa kila aina ya matumizi ya mitandao. Hii ni pamoja na kuwa na nywila thabiti, kuepuka viunganishi hatarishi, kuripoti majaribio la ulaghai, kutumia namba rasmi za huduma kwa wateja wa mitandao husika na umakini kwenye miamala ya kifedha.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt Jabiri Bakari amesema wataendelea kuwachukulia watoa huduma ambao mitandao yao inatumiwa kwa ulaghai ikiwa ni pamoja na hatua za kiudhibiti na kikanuni. TCRA pia inatoa elimu kwa watumiaji na umma kwa ujumla kuhusu namna ya kujilinda mitandaoni.

Wananchi na watumiaji wanakumbushwa kutumia nywila thabiti na tofauti kwa kila akaunti, kutokufuata maelekezo na kutoa nywila au namba yako ya uthibitisho kwa mtu yeyote na kuepuka kubofya viunganishi (link) wasivyovifahamu.

Elimu hiyo pia inasisitiza umakini wa watumiaji wanapofanya miamala ya kifedha.

**HAKIKI NAMBA YAKO KUPITIA**

***106#**

**RIPOTI UTAPELI: TUMA UJUMBE BILA MALIPO**

**15040**

Mhe. Waziri amepongeza watoa huduma waliofanikiwa kwenye hatua walizochukua kudhibiti usajili na matumizi ya laini zinazohusika kwenye ulaghai.

**Jedwali: Matukio ya majaribio ya ulaghai yaliyoripotiwa kwa kila robo mwaka kuanzia Oktoba 2022**

| Robo mwaka | Matukio | Kuongezeka, kupungua | Asilimia ya kuongezeka, kupungua | Mikoa inayoongoza (asilimia ya matukio yote) |
|---|---|---|---|---|
| Oktoba – Desemba 2022 | 12,613 | NA | NA | Rukwa 46%<br>Morogoro 25% |
| Januari –Machi 2023 | 12,044 | ▼ Pungua (596) | 5% | Rukwa 45%<br>Morogoro 18% |
| Aprili – Juni 2023 | 23,048 | ▲ Ongezeka 11,044 | 48% | Rukwa 46%<br>Morogoro 25% |
| Julai – Septemba 2023 | 23,328 | ▲ Ongezeka 280 | 1% | Rukwa 36%<br>Morogoro 28% |
| Oktoba – Desemba 2023 | 20,939 | ▼ Pungua (2,389) | 10% | Rukwa 33%<br>Morogoro 29% |
| Januari – Machi 2024 | 23,328 | ▼ Pungua (3,621) | 17% | Rukwa 36%<br>Morogoro 28% |
| Aprili –Juni 2024 | 22,287 | ▲ Ongezeka 4,969 | 29% | Rukwa 33%<br>Morogoro 29% |
| Julai – Septemba 2024 | 16,069 | ▼ Pungua (6,218) | 28% | Rukwa 35%<br>Morogoro 34% |
| Oktoba – Desemba 2024 | 12,896 | ▼ Pungua (3,173) | 30% | Rukwa 41%<br>Morogoro 33% |

Muhtasari: Matukio ya ulaghai yalipungua kidogo robo mwaka ya Oktoba-Desemba 2022 kutoka 12,613 hadi 12,044 Januari Machi 2023. Yaliongezeka na kufikia 23,329 Julai-Septemba 2023 na kushuka hadi 17,318 Januari -Machi 2024. Hata hivyo yaliongezeka tena na kufikia 22,287 Aprili –Juni kabla ya kuanza kupungua hadi 12,896 Oktoba-Desemba.

Ulaghai umeongezeka mkoani Morogoro kutoka asilimia 28 ya matukio kitaifa Julai—Septemba 2023 kufikia asilimia 33 Oktoba Desemba mwaka jana. Pamoja na Rukwa na Morogoro kuwa vinara wa uhalifu kwenye mitandao ya simu wilaya ya Kilombero mkoani Morogoro ina asilimia 32 ya matukio ya majaribio ya uhalifu. Kati ya hayo matukio 12,896 ya Oktoba hadi Desemba, Kilombero ilikuwa na 4,101.

Matukio Kilombero yameongezeka kwa asilimia 214, kutoka 1,306 Septemba 2024.

Mawasiliano Towers,
20 Sam Nujoma Road,
14414 Dar es Salaam, Tanzania.
Email: dg@tcra.go.tz

@tcra_tanzania